JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA

MAELEZO KUHUSU WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA

Majukumu, Mafanikio, Changamoto na Mikakati (2011-2015)

Januari, 2016

YALIYOMO ..... Error! Bookmark not defined.
1. UTANGULIZI 1
1.1 Maelezo ya Jumla 1
1.2 Lengo Kuu la Kuanzishwa TFS 1
1.3 Dira 2
1.4 Dhima 2
1.5 Maadili makuu 2
1.6 Majukumu Makuu ya Wakala 2
2. MAFANIKIO MAKUU TANGU KUANZISHWA WAKALA 2
2.1 Kujenga na Kuimarisha Mifumo ya Kiutendaji ya Taasisi 3
2.2 Kuanzisha na Kusimamia Misitu ya Hifadhi na Hifadhi za Nyuki za Serikali kuu 4
2.3 Kuboresha Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali 5
2.3.1 Mapato na Vyanzo Vyake 5
2.3.2 Mambo Yaliyochangia Kuongezeka kwa Ukusanyaji Maduhuli 11
2.3.3 Mgawanyo wa Maduhuli 12
2.3.4 Maelezo ya Maduhuli yaliyobaki TFS 15
2.3.5 Ubunifu na Mikakati ya Kuongeza Mapato ya Wakala 15
3. MWENENDO WA MATUMIZI KATIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YA WAKALA 16
3.1. Mwenendo wa Matumizi Kwa Kila Lengo Kuu (Objective) 16
3.2. Ubunifu na Mikakati ya Udhibiti wa Matumizi 18
4. UTAWALA BORA NA JINSIA 18
5. KUPAMBANA NA JANGA LA UKIMWI NA KUTOA HUDUMA KWA WATUMISHI WANAOISHI NA HIV/AIDS 19
6. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA 19
7. MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO 19
8. MIPANGO YA BAADAYE YA WAKALA 19

1. UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Jumla

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (Tanzania Forest Services Agency) ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala; *the Executive Agencies Act Cap. 245 (Revised Edition 2009)***,** kutangazwa katika Gazeti la Serikali (GN 269) la Julai 30, 2010 na kuzinduliwa Julai 18, 2011. Kuanzishwa kwa TFS kumezingatia pia Sera za Taifa za Misitu na Ufugaji Nyuki za 1998, na Sheria za Misitu na Nyuki Sura 323 na Sura 224 za 2002.

Wakala huu uliundwa chini ya Programu ya Serikali ya Maboresho katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2000 (*Public Service Reforms Programme (PSRP 2000*)). Programu hii ililenga kuimarisha Idara na Wakala wa Serikali (*Ministerial Departments & Agencies (MDAs*)) kutoa huduma bora za kiutendaji zaidi katika utumishi wa umma. Kiutendaji Wakala unatekeleza majukumu yaliyokuwa ya Idara ya Misitu na Nyuki isipokuwa utungaji wa sera, sheria na programu za sekta za misitu na nyuki na kusimamia vyuo vya mafunzo ya misitu na nyuki.

Wakala umekabidhiwa kusimamia rasilimali za misitu na nyuki zenye ukubwa hekta milioni 16.65 (40%) kati ya eneo lote la misitu hektari millioni 48.1 au (55%) ya eneo la Tanzania Bara (millioni 88.6). Muhutasari wa umiliki wa ardhi yenye misitu umeooneshwa kwenye **Jedwali Na. 1**.

Jedwali Na. 1: Umiliki wa Ardhi yenye Misitu

Umiliki wa Rasilimali Misitu	**Eneo (Milloni Ha)**	**Asilimia**
Serikali Kuu (Forest and Wildlife reserves)	16.835	35
Serikali za Mitaa	3.367	7
Serikali za Vijiji	21.645	45
Sekta Binafsi	3.367	7
Ardhi yenye misitu isiyohifadhiwa chini ya TFS	2.405	5
Nyingine	0.481	1
Jumla	**48.1**	**100**

Kimuundo Wakala umegawanyika katika ngazi kuu nne ambazo ni: Makao Makuu, Kanda na Mashamba ya miti na Wilaya. Menejimenti ya Wakala inajumuisha Mtendaji Mkuu, Wakurugenzi watatu (Usimamizi wa Maendeleo ya Rasilimali, Mipango na Matumizi ya Rasilimali na Huduma za Uendeshaji), Meneja wa Vitengo vya Sheria na Ugavi, Mhasibu Mkuu na Mkaguzi Mkuu wa Ndani. Wakala una kanda saba (7) na mashamba ya miti 18 na kila kanda au shamba huongozwa na meneja. Aidha, kati ya wilaya 169 za Tanzania Bara wilaya 133 zina meneja wa TFS.

1.2 Lengo Kuu la Kuanzishwa TFS

Lengu Kuu la kuanzishwa kwa Wakala wa Huduma za Misitu ni kuhakikisha uwepo wa usimamizi madhubuti, wenye ufanisi na tija wa rasilimali za misitu na nyuki; kuongeza thamani ya mazao ya misitu na nyuki na kutoa huduma bora kwa umma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa umma.

1.3 Dira

Kuwa kielelezo bora katika usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu na nyuki.

1.4 Dhima

Kuwa na usimamizi endelevu wa rasilimali za taifa za misitu na nyuki ili kuchangia kikamilifu mahitaji ya kijamii, kiuchumi, ki-ikolojia na kiutamaduni kwa kizazi cha sasa na kijacho.

1.5 Maadili makuu

Wakala unaongozwa na maadili makuu yafuatayo:
Kuzingatia weledi, Uwazi na uwajibikaji, Uadilifu, Ufanisi na ufasaha, Kutunza siri Kutoa huduma bora, Ubunifu wenye kuleta mabadiliko chanya, Kufanya kazi kwa ushirikiano.

1.6 Majukumu Makuu ya Wakala

Wajibu na majukumu ya TFS yameainishwa kwenye "**Establishment Order (GN No 269)"** ya tarehe 30 Julai 2010. Wakala una majukumu makuu yafuatayo:

a) Kuanzisha na kusimamia Misitu ya Hifadhi na Hifadhi za Nyuki za Serikali kuu;
b) Kuanzisha na kusimamia mashamba ya miti na manzuki za Serikali kuu;
c) Kusimamia rasilimali za misitu na nyuki katika ardhi ya jumla (General Land);
d) Kusimamia utekelezaji wa Sheria za Misitu na Ufugaji Nyuki katika maeneo yaliyo chini ya Wakala;
e) Kukusanya Maduhuli yatokanayo na mazao ya misitu;
f) Kutoa huduma za ugani katika maeneo ya Wakala;
g) Kufanya biashara ya mazao na huduma za Misitu na Ufugaji Nyuki;
h) Uperembaji na tathimini kuhusu utekelezaji wa kazi za Wakala.

2. MAFANIKIO MAKUU TANGU KUANZISHWA WAKALA

Mafanikio ya Wakala yamepatikana kupitia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa kwanza wa miaka mitatu (2011-20014) na sasa Wakala unatekeleza Mpango Mkakati wa pili wa miaka mitano (2014-2019).

Kuna Malengo Makuu (Objectives) tano katika Mpango Mkakati wa wakala ambayo yanaaisha Malengo matatu yanayolenga majukumu ya msingi (core functions) na Malengo mawili yanayohusu masuala mtambuka. Majukumu ya msingi yanatekelezwa na Malengo matatu ambayo ni:

a) Kuimarisha uwezo wa taasisi kutoa huduma kwa umma (Institutional capacity to deliver services stregthened).

b) Kuhakikisha upatikanaji wa mazao bora ya misitu na nyuki (Sustainable supply of quality forest and bee products enhanced).

c) Kuimarisha mifumo ikolojia na bionuwai (Stable ecosystem and biological diversity maintained).

Masuala mtambuka hutekelezwa kupitia Malengo Makuu mawili ambayo ni:

(i) Kupunguza maambukizi ya VVU na kuboresha huduma kwa wathirika wa VVU (HIV/AIDS infections reduced and supportive services to people living with HIV/AIDS improved).

(ii) Kuboresha masuala ya utawala bora na jinsia (Good governance and gender balance enhanced).

Kufuatana na Malengo Makuu (Objectives) utekelezaji wa Mpango Mkakati, mafanikio yamegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo:

2.1 Kujenga na Kuimarisha Mifumo ya Kiutendaji ya Taasisi

a) Kuanzisha na kuimarisha Kanda saba za Wakala ili kuleta ufanisi na tija katika kutekeleleza majukumu ya uhifadhi na usimamizi misitu nchini. Wakala umeanzisha ofisi na kuwa watumishi katika Wilaya 133 kati ya wilaya 169 nchini. Aidha Wakala umeongeza rasilimali watu wa kada mbalimbali ya kusimamia rasilimali za misitu na nyuki kutoka watumishi 1,469 mwaka 2010/2011 hadi kufikia watumishi 2,072 mwaka 2014/2015 sawa na ongezeko la watumishi 880 wa kada mbalimbali. Wakala ulirithi watumishi 1469 wa kada mbalimbali kutoka Idara ya Misitu na Nyuki (**Kiambatisho Na. 1**).

b) Kuwa na Mifumo na Mwongozo wa Utendaji Kazi, Hati ya Kuanzisha Wakala , Mpango Mkakati, Mpango wa Biashara wa Mwaka, Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS), Uperembaji na Tathmini, Mkataba wa Huduma kwa Mteja na Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko. Aidha mifumo mingine inayotumiwa na Wakala kutekeleza majukumu yake ni Mfumo wa Usimamizi na Uhakiki wa Fedha (Integrated Financial Management System (IFMS)), Human Capital Information Management System, Masjala na Uhasibu.

c) Wakala umeandaa Muundo wa Utumishi (Schemes of Service) ambao ulipitishwa kwa ajili ya kuanza kutumika mwaka wa fedha 2016/2017, pamoja na kupatiwa Kasma (Vote) yake Namba TR 47. **Muundo huu mpya una kada ya "Forest Guards".**

d) Wakala umejenga majengo 18 katika mashamba ya miti, barabara mpya za msituni za kilomita 277.8na kukarabati kilomita 11,536.21, madaraja 55 na mnara mmoja.

e) Vitendea kazi: Wakala umeendelea kuboresha vitendea kazi ilivyorithi kutoka Idara ya Misitu na Nyuki kwa kukarabati na kununua vingine kulingana na Mipango kazi ya utekelezaji kwa kila mwaka tangu kuanzishwa kwake. Wakala umefanikiwa kununua magari-4WD **47, malori 10, pikipiki 300, mitambo mikubwa (motor grader 1, Minibus 2, Wheel loader 1 na soil compactor 1)** na vifaa vingine kama vilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na.2**.

2.2 Kuanzisha na Kusimamia Misitu ya Hifadhi na Hifadhi za Nyuki za Serikali kuu

a) Takwimu za Misitu kwa ajili ya mipango endelevu na kufanya maamuzi sahihi.

Tathmini za Rasilimali za Misitu (National Forest Resource Monitoring and Assessment (NAFORMA imefanyika na kutoa takwimu sahihi za rasilimali za misitu nchini zitakazotumika katika kufanya maamuzi sahihi ya jinsi ya kusimamia rasilimali hizo kiuendelevu. Taarifa ya NAFORMA inapatikana katika tovuti ya Wakala (www.tfs.go.tz). Aidha, takwimu hizi zinawezesha kutoa taarifa katika Mifumo ya Kimataifa kuhusu hali ya misitu Tanzania.

b) Uendelezaji wa Mashamba ya Miti na Kuongoa maeneo yaliyoharibika

Pamoja na kurithi mashamba 14 kutoka Idara ya Misitu na Nyuki, Wakala umeanzisha mashamba manne hivyo kufikisha mashamba 18 yenye eneo la hekta 284,549.85 kati hizo, hektari 96,500 zimepandwa miti.

Kwa kipindi cha miaka minne, Wakala imeongeza kasi ya upandaji miti kutoka hekta 1,275 kwa mwaka hadi hekta 8,000 kwa mwaka. Katika kipindi cha miaka mitano, Wakala umeweza kupanda jumla ya hekta39,776 katika mashamba yake, ambapo Hekta 24,695.5zilirudishiwa kupandwa miti baada ya kuvunwa na hekta 15,080.5 ni upandaji katika maeneo mapya. Wakala umetayarisha Mipango ya Usimamizi katika mashamba yote 18 ya miti.

JEDWALI Na. 2: Upandaji Miti kwenye Mashamba

Mwaka	Maeneo Yaliyovunwa (Ha)	Maeneo Mapya (Ha)	Jumla (Ha)
2010/11	6,897.00	949.20	7,846.20
2011/12	5,383.00	2,673.00	8,056.00
2012/13	4,653.30	3,006.30	7,659.60
2013/14	4,219.00	3,745.00	7,964.00
2014/15	**3,543.20**	4,707.00	8,250.20
JUMLA	**24,695.50**	**15,080.50**	**39,776.00**

Aidha, miche ya miti ya aina mbalimbali imepandwa katika jumla ya hekta 210 za maeneo ya misitu yaliyoharibika (degraded forests).

c) Kuimarisha mipaka ya Hifadhi za misitu na nyuki

Kazi ya kuimarisha mipaka ya hifadhi 235 (51.64%) kati ya misitu ya hifadhi 455 ya TFS imefanyika ili kuzuia uvamizi wa misitu kwa ajili ya makazi, kilimo na ufaugaji. Sorovea na kusafisha mipaka yenye urefu wa kilomita 14,834 vimefanyika katika

misitu ya asili ya hifadhi ya kuvunwana isiyoyakuvunwa.Vilevilemaboya 3,006 (beacons), vibao vya alama 4,728 (sign boards), mashimo ya mwelekeo 1,053 (directional trenches) na kupandamiti kwenye mpaka wa urefu wa kilomita 127 vimetekelezwa. Aidha, ramani 40 za misitu ya hifadhi na ramani 3 za hifadhi za nyuki zinazopendekezwa ulifanyika.

d) Kuboresha Ufugaji Nyuki

Jumla ya manzuki 21 zenye mizinga 3,870 zilisimamiwa na hekta 69,613 za hifadhi za nyuki zimependekezwa. Wakala uligawa mizinga 14,076kwa vikundi na wadau mbalimbali. Aidha, wilaya 29 na mashamba ya miti 7 zimeanzisha manzuki 36 na kutundika mizinga 4,184.

Vilevile Wakala umefanikiwa kuanzisha Chama cha kuendeleza ufugaji nyuki Tanzania.Chama hiki kinaunganisha wafugaji nyuki wote nchini

e) Kuimarisha ulinzi wa misitu

Wakala uliweza kufanya doria ya jumla ya siku za doria 399,464 katika maeneo inayoyasimamia ambapo ilikamata mbao 295,508; magunia ya mkaa 97,451; milango 1,380; magogo 13,983; nguzo 148,397;na wahalifu 132 walikamatwa (kesi 60 zipo mahakamani).

f) Usimamizi misitu

(i) Wakala umetayarisha Mpango bora wa usimamizi na uhifadhi wa misitu, na moja ya mikakati iliyopo kwenye mpango huo ni kupanda hekta 185,000 za miti kwa mwaka kwa kushirikiana na wadau ili kuziba pengo la mita za ujazo 19.5 milioni kwa mwaka za timbao hadi kufikia mwaka 2030.

(ii) Wakala umeimarisha usimamizi shirikishi wa misitu (Participatotry Forest Management-PFM) ambapo Mwongozo wa kugawana majukumu na manufaa umetayarishwa na kukubaliwa na wadau. Vijiji 163 vimefundishwa jinsi ya kushiriki katika usimamizi wa pamoja na jumla ya hekta 7.7 milioni zimewekwa katika usimamizi uliojikita kwa jamii.

(iii) Wakala umetoa elimu ya uhifadhi katika jumla ya vijiji 1,872 na kuwasomesha watumishi 523.

2.3 Kuboresha Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali

2.3.1 Mapato na Vyanzo Vyake

Jumla ya TSh **303,831,222,078** zilikusanywa na TFS katika kipindi cha miaka minne (2011/12 – 2014/2015). Kufuatana na Taarifa za Fedha (Financial Statements) kwa

miaka minne (2011/12 – 2014/2015), zinaonesha Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania umekusanya jumla ya **TSh 293,501,326,391.** Mapato haya ni mafanikio ya asilimia 106 ya jumla ya lengo la maotea ya **TSh 278,696,117,456** kwa kipindi cha miaka minne. Taarifa hizo za fedha hazijajumuisha **TSh 10,620,931,746** zilizokusanywa kama VAT na CESS kwa miaka ya 2011/12 na 2012/13.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16 hadi Disemba 13, 2015, Wakala umefanikiwa kukusanya **TSh 44,079,623,078.77** ambazo ni sawa na 99.42% ya maoteo ya **TSh 44,337,146,000** ya kipindi cha Julai – Disemba 2015. Mwenendo huu unaashiria kuweza kufika malengo ya nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2015/16. Hivyo, jumla ya mapato halisi yaliyokusanywa hadi Disemba 13, 2015 ni **TSh 334,199,799,298.** Mapato haya hukusanywa kama mrahaba na ada mbalimbali za mazao na huduma za misitu na nyuki. Aina ya zao na huduma pamoja na chanzo chake vimeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 2.**

Jedwali Na. 2: Aina ya mazao na Huduma za misitu na nyuki na vyanzo vyake

S/N	**Zao/ Huduma**	**Chanzo**
1	Magogo na Veneer	Mashamba ya Miti, Misitu ya Asili – ilioyohifadhiwa na ile ya ardhi huria
2	Nguzo	Mashamba ya Miti, Misitu ya Asili – ilioyohifadhiwa na ile ya ardhi huria
3	Kuni na Mkaa (Wood fuel)	Mashamba ya Miti, Misitu ya asili
4	Utalii ekojia (Ecotourism)	Mashamba ya miti, Hifadhi za misitu ya asili ikihusisha misitu ya hifadhi asilia na misitu ya Mikoko
5	Maeneo ya kufanyia tafiti na materials	Mashamba ya miti, na Misitu ya asili pamoja na misitu ya hifadhi asilia (nature reserves)
6	Maeneo kwa ajili ya minara ya simu	Misitu ya Maeneo ya Miinuko (Mountainous) forests
7	Uchimbaji madini	Misitu ya hifadhi
8	Mitishamba (Medicinal plants)	Mashamba na Misitu ya Asili
9	Usajili wa wafanyabiashara	Wafanya biashara mazao ya misitu
10	Mazao ya Nyuki (honey & bees wax)	mashamba ya miti na misitu ya asili
11	vibali vya kuingiza na kusafirisha mazao ya misitu ndani na nje (Export and import permits)	Wafanyabiashara
12	Fomu za maombi na kibali cha kusafirishia mazao ya misitu	wawekezaji na wafanya biashara
13	Logging and Miscellaneous Deposit Account (LMDA)	Mashamba ya miti

Jedwali Na. 3 linaonesha mchanganuo wa makusanyo kulingana na vyanzo mbalimbali kama ilivyooneshwa kwenye Taarifa za Fedha (Financial Statements).

Aidha, Taarifa za Fedha (Audited Financial Statements) katika mwaka wa fedha 2011/12 na 2012/13 hazikujumuisha makusanyo ya VAT na CESS ingawa takwimu zake zilipatikana kutoka vituo vinavyokusanya.

Jedwali Na. 3: Maduhuli yaliyokusanywa na Wakala yaliyokusanywa kwa Kila Chanzo kwa Miaka Minne Kufuatana na Taarifa za Fedha (Audited Financial Statements)

(2011/2012 -2014/2015)

Kifungu Na.	Maelezo	Makusanyo kwa Mwaka (TSh)				Jumla
		2011/2012	2012/2013	2013/2014	2014/2015	
110620	Forestry Export Certificate and import Permit	313,324,005	621,284,814	522,553,924	586,893,517.49	**2,044,056,260**
140112	Rent – Telecommunication tower	-	18,885,000	14,000,000	41,815,620.00	**74,700,620**
140354	Forestry Royalties	45,719,098,965	39,648,773,868	40,689,419,558	61,357,266,744.13	**187,414,559,135**
140313	Receipts from Registration fees	811,004,567	1,525,584,438	5,496,468,022	1,864,142,268.51	**9,697,199,296**
140340	Receipts from compounding fees	95,905,585	1,221,899,993	747,786,616	320,473,222.00	**2,386,065,416**
140347	Exploration/Mining	-	11,748,000	2,108,000	347,137,120.00	**360,993,120**
140261	Receipts from Honey and bees wax	6,907,200	7,180,060	21,162,616	9,908,939.00	**45,158,815**
140357	Receipts from Sale of Confiscated Forest Products		21,888,954	374,894,437		**396,783,391**
140365	Receipts from Recovery of stores	-	4,355,750	58,000		**4,413,750**
140345	Receipts from Transit Pass fees		320,209,965	2,807,170,824	566,693,782.25	**3,694,074,571**
140344	Receipts from Entrance fee to Natural Forests		21,375,690	4,164,800	54,514,347.00	**80,054,837**
140346	Receipts From Camping fee to Nature Reserves		101,493,765	3,130,674	18,444,756.00	**123,069,195**
140370	Recovery of Public money			100,000	98,000.00	**198,000**
140283	Receipts from Sale of Tender Documents		1,250,000	3,700,000	4,475,000.00	**9,425,000**

Kifungu Na.	Maelezo	Makusanyo kwa Mwaka (TSh)				Jumla
		2011/2012	2012/2013	2013/2014	2014/2015	
140343	Receipts from Research Fees			39,807,460	20,346,511.00	**60,153,971**
140368	Miscellaneous Receipts	2,292,399,589	602,847,082	7,514,693,226	402,510,613.78	**10,812,450,511**
	Unsubmitted document		3,205,539,771			**3,205,539,771**
	Upcountry Collection Accounts untransfered		704,122,500			**704,122,500**
	Inspection fee	-			72,000.00	**72,000**
	Road fee				2,180,010.00	**2,180,010**
	Application form for harvesting licence				152,571,799.00	**152,571,799**
	Jumla ndogo	**49,238,639,911**	**48,038,439,650**	**58,241,218,157**	**65,749,544,250**	**221,267,841,969**
	LMDA (a)	11,174,962,860	11,732,889,363	12,636,282,939	13,447,101,199.65	**48,991,236,362**
	TaFF (b)	3,338,883,101	3,188,309,104	2,690,345,278	3,152,945,078.87	**12,370,482,562**
	CESS (c)			698,785,333	862,509,412.35	**1,561,294,745**
	VAT (d)			4,250,808,177	5,059,662,576.02	**9,310,470,753**
	Jumla ndogo ((a) – (d))	**14,513,845,961.00**	**14,921,198,467.00**	**20,276,221,727.00**	**22,522,218,266.89**	**72,233,484,422**
	JUMLA KUU	**63,752,485,872.00**	**62,959,638,117.00**	**78,517,439,884.49**	**88,271,762,517.05**	**293,501,326,391**

NB: Kufuatana na taarifa zilizopokelewa kutoka vituoni, jumla ya Shs 9,094,941,640 zilikusanywa kama VAT na TSh 1,525,990,106 zilikusanywa kama CESS kwa miaka ya 2011/12 na 2012/13 kama ilivyooneshwa hapo chini.

AINA/MWAKA	2011/12	2012/13	Jumla
VAT (TSh)	4,123,806,388	4,971,135,252	**9,094,941,640**
CESS (TSh)	655,118,427	870,871,679	**1,525,990,106**
Jumla (TSh)	**4,778,924,815**	**5,842,006,931**	**10,620,931,746**

2.3.1 Mwenendo wa Maduhuli kabla na baada ya kuanzishwa Wakala

Ukusanyaji maduhuli yanayotokana na mazao ya misitu na huduma unaonekana kuongezeka kwa kasi hasa baada ya kuanzishwa kwa Wakala. **Jedwali Na. 4** linaonesha makadirio na makusanyo halisi ya makusanyo kwa kipindi cha miaka 10. Miaka mitano ya utekelezaji wa Idara ya Misitu na Nyuki (FBD) na miaka minne ya utekelezaji wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (**Kielelezo Na. 1**).

Jedwali Na. 4: Maoteo na Makusanyo ya Maduhuli kwa kipindi cha miaka kumi (2005/2006 – 2015/2016)

Taasisi	Mwaka	Maoteo (TSh)	Ukusanyaji Halisi (TSh)	Asilimia ya makusanyo
FBD[1]	2005/06	10,106,150,000	10,961,257,440	108
FBD	2006/07	11,898,002,000	15,558,990,053	131
FBD	2007/08	15,601,740,000	26,447,226,072	170
FBD	2008/09	23,673,889,000	25,166,959,462	106
FBD	2009/10	23,825,361,000	28,406,865,318	119
FBD/TFS	2010/11	54,704,086,834	39,258,242,578	72
TFS	2011/12	54,156,486,816	63,752,485,873	118
TFS	2012/13	75,137,556,879	62,668,602,056	83
TFS	2013/14	68,173,076,760	80,441,400,451	118
TFS	2014/15	81,228,596,000	88,271,762,517	109
TFS	2015/16[2]	87,596,411,000	44,079,623,078.77.[3]	50.32

[1] FBD – Forest and Beekeeping Division ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii

[2] Kipindi cha miezi 6 (Julai – Desemba, 2015)

[3] Makusanyo hadi Disemba 28, 2015



Kielelezo Na.1: Mwenendo wa ukusanyaji maduhuli kabla na baada ya TFS

2.3.2 Mambo Yaliyochangia Kuongezeka kwa Ukusanyaji Maduhuli

Jitihada mbalimbali zimefanywa na Wakala kuongeza mapato, kama ilivyooneshwa katika taarifa hii. Ongezeko hili limeonekana kwa kiasi kikubwa baada ya kuanzishwa kwa Wakala katika kipindi cha mwaka 2011/12 hadi sasa. Mambo yaliyochangia kuongezeka kwa mapato hayo ni pamoja na:

a) Kufanya mapitio ya viwango vya tozo ya mazao na huduma za misitu kila baada ya miaka miwili. Katika kutekeleza hili TFS kupitia Wizara ilitoa Tangazo la Serikali (GN) kwa vipindi vya mwaka 2011 kwa **GN 432/2011**; mwaka 2013 **GN 433/2013** na mwaka 2015 **GN 324/2015**. Mapitio haya yalifanyika yakizingatia gharama za kuanzisha na kuendeleza mashamba ya miti pamoja na usimamizi wa misitu yote kwa ujumla, hali/mwenendo wa soko la mazao ya misitu na kwa kuzingatia mfumuko wa bei (inflation). Viwango hivyo viliongezwa kwa kiasi cha kati ya 10% na 28% kila ilipofanyika mapatio ya Tangazo la Serikali kwa kuzingatia utafiti uliofanyika kabla ya kubadili viwango vya mrahaba na ada.

b) Uuzaji wa miti ya mitiki kwa njia ya minada (Auction) na makubaliano (Private Agreements) kwa kuzingatia Kanuni za Misitu za mwaka 2004. Utaratibu huu

umeongeza ushindani na kuongeza bei ya soko hivyo kuongeza mapato kwa Wakala.

c) Kuajiri na kutawanya watumishi katika vituo hivyo kuchangia kuimarisha usimamizi misitu na udhibiti wa uvujaji wa mapato na rasilimali za misitu na nyuki.

d) Kuvuna miti katika mashamba kwa kuzingatia mpango wa uvunaji wa mashamba na kupata kiasi cha ujazo wa miti kinachostahili kuvunwa kwa mwaka, na kuuza kwa bei ya soko. Hali hiyo ilichangia upatikanaji wa maduhuli yanayotarajiwa.

e) Kufanya doria za kupanga na kushitukiza katika maeneo ya misitu, barabarani mipakani, baharini na sehemu za biashara;

f) Kufanya ukaguzi wa kawaida na wa kushitukiza katika vituo vya ukusanyaji wa maduhuli ili kubaini kama sheria na taratibu za fedha na biashara ya mazao ya misitu na nyuki zinazingatiwa.

g) Kuongeza vitendea kazi hivyo kuleta ufanisi katika kusimamia ukusanyaji wa maduhuli na uhifadhi wa rasimali misitu na nyuki.

h) Kuimarisha usimamizi wa uvunaji katika misitu ya asili kwa kupitia Kamati za uvunaji za Wilaya.

i) Kutoa elimu na kuongeza uelewa wa wadau kuhusu sheria, kanuni na taratibu za biashara ya mazao na huduma za misitu.

2.3.3 Mgawanyo wa Maduhuli

Jumla ya TSh **303,831,222,078** zilikusanywa na TFS katika kipindi cha miaka minne (2011/12 – 2014/2015). Mapato haya yaligawanywa kwa kuzingatia Sheria ya Wakala Sura 245, Sheria ya Misitu Na 14 na Sheria ya Ufugaji Nyuki Na 15, Establishment Order No 269, Waraka wa Hazina (Treasury Circular) Namba 6 wa 2011/12 na Sheria nyingine pamoja na Mpango wa Kibiashara wa TFS wa kila mwaka.

Hivyo, mapato yaligawanywa kwa ajili ya kugharamia shughuli za Wakala kulingana na Mpango wa Kibiashara; Kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina kupitia Wizara; Mfuko wa Misitu Tanzania uliopo chini ya usimamizi wa Wizara; Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) chini ya TRA; na Ushuru wa Halmashuri za Wilaya (CESS).

Katika kipindi miaka minne (2011/12 hadi 2014/15, jumla ya **TSh 111,529,122,828** (36.71%) zimewasilishwa Hazina kupitia Wizara; Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) uliopo chini ya Wizara **TSh 12,370,482,561 (4.07%);** Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kama kodi ya ongezeko la thamani (VAT) TSh **18,405,412,393 (6.06%);** na Halmashauri za Wilaya TSh **3,087,284,851 (1.02%)** na Taasisi chini ya Wizara

(TAWIRI, FTI, FITI na BTI)[4] **TSh 2,506,612,500 (0.83%)** Aidha, jumla ya TSh **155,932,306,945 (51.32%)** ya mapato yote **TSh 303,831,222,078** yalitumika kugharamia kazi za Wakala ikijumuisha kuendeleza mashamba ya miti na kusimamia misitu ya asili na ufugaji nyuki. **Jedwali Na. 5** linaonesha mgawanyo wa mapato yaliyokusanywa na TFS.

[4] TAWIRI = Tanzania Wildlife Research Institute

FTI = Forestry Research Institute

FITI = Forestry Industries Training Institute

BTI = Beekeeping Training Insitute

Jedwali Na. 5: Mgawanyo wa Mapato yaliyokusanywa na TFS (2011/12 – 2014/15)

Eneo la mgawanyo wa maduhuli/ Mwaka	**2011/2012**	**2012/2013**	**2013/2014**	**2014/2015**	**Jumla (TSh.)**	**%**
Mapato yaliyowasilishwa Hazina kupitia MNRT (TSh)	31,074,228,042	20,454,894,786	30,000,000,000	30,000,000,000	**111,529,122,828**	**36.71**
Mapato yaliyowasilishwa Mfuko wa Misitu Tanzania (TSh)	3,338,883,101	3,188,309,104	2,690,345,277	3,152,945,079	**12,370,482,561**	**4.07**
Mapato yaliyowasilishwa TRA (VAT (TSh)	4,123,806,388	4,971,135,252	4,250,808,177	5,059,662,576	**18,405,412,393**	**6.06**
Mapato yaliyowasilishwa H/Wilaya (CESS (TSh)	655,118,427	870,871,679	698,785,333	862,509,412	**3,087,284,851**	**1.02**
Mapato yaliyowasilishwa Taasisi chini ya Wizara (TAWIRI, FTI, FITI na BTI) (TSh)	796,612,500	607,500,000	480,000,000	622,500,000	**2,506,612,500**	**0.83**
LMDA (Mashamba ya miti) (TSh)	11,174,962,860	11,732,889,363	12,636,282,939	13,447,101,200	**48,991,236,362**	**16.12**
Makusanyo yaliyobaki TFS (TSh)	17,367,799,370	26,685,008,803	27,761,218,159	35,127,044,250	**106,941,070,582**	**35.20**
Jumla ya Mapato (TSh)	**68,531,410,689**	**68,510,608,987**	**78,517,439,885**	**88,271,762,517**	**303,831,222,078**	**100.00**

2.3.4 Maelezo ya Maduhuli yaliyobaki TFS

Jedwali Na 5 la mgawanyo wa maduhuli linaonesha Wakala umepata TShs **155,932,306,944** katika kipindi cha miaka minne Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 51.3** ya maduhuli yote. Fedha hizo zinatokana na Tozo la kuendeleza Mashamba ya Miti (LMDA Tshs 48,991,236,362) na sehemu ya mrahaba na ada za mazao ya misitu na nyuki (Tsh 106,941,070,582.87). Maduhuli hayo yametumika kugharamia shughuli mbalimbali za msingi za TFS (core functions) katika kuhifadhi, kusimamia rasilimamili za misitu na nyuki ikiwa pamoja na kuendeleza mashamba ya miti.

Wakala umeendelea na utaratibu wa kukusanya fedha kwa ajili ya uendelezaji wa mashamba ya miti (LMDA), hasa katika shughuli za ustawishaji, ujenzi na ukarabati wa barabara za msituni. Fedha hizi ambazo zinabaki katika akaunti za mashamba zinatumika kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa. Mashamba matatu (3) yaani Sao Hill, Meru/USA na North Kilimanjaro (Rongai) kati ya mashamba ya miti 18 ya Wakala yanakusanya fedha (LMDA) inayokidhi bajeti yake na mashamba mengine yanakusanya pungufu kutokana na kuwa na ujazo mdogo wa miti iliyokomaa kwa kuvunwa.

Mashamba yenye upungufu/yanayokusanya LMDA isiyokidhi bajeti yake na yale ambayo hayana uvunaji ni mashamba mapya ya Ruvu, Wino, Mbizi na Korogwe na mashamba yenye uvunaji mdogo na yasiyovuna ambayo ni Buhindi, Kawetire, Kiwira, Longuza, Mtibwa, Rondo, Rubare, Rubya, Shume, Ukaguru na West Kilimanjaro. Mashamba haya 15 yanatengewa au kuongezewa bajeti katika fedha zinazotoka katika vyanzo vingine/mashamba mengine na kutumiwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kuendeleza mashamba.

2.3.5 Ubunifu na Mikakati ya Kuongeza Mapato ya Wakala

Pamoja na ufanisi uliooneshwa na Wakala katika ukusanyaji wa maduhuli, Wakala una fursa zaidi ya kuongeza mapato yake. Mikakati kadhaa imeandaliwa kwa ajili ya kuongeza ukusanyaji wa maduhulio hayo na kuendelea kuziba mianya ya uvujaji wa mapato. Mikakati ifuatayo imeandaliwa:

a) Kufuatilia mwenendo wa mapato ya kila wiki kutoka kila kituo;
b) Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika vituo vya kukusanyia mapato ya Wakala;
c) Kutoa maelekezo ya mara kwa mara ya namna bora ya ukusanyaji na uwasilishaji wa maduhuli yanayokusanywa.
d) Ukusanyaji wa mapato ya Wakala kwa njia ya ki-electronic.
e) Kufanya uperembaji kwa kila robo mwaka;
f) Kuongeza watumishi wa kada ya 'Walinzi wa misitu' (Forest Guards) katika Muundo wa Utumishi wa Wakala; hivyo kuímarisha udhibiti na usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki na kupunguza mianya ya upotevu wa mapato;

g) Kufanya mzunguko wa mara kwa mara wa watumishi wanaokaa katika vituo vya kukusanyia mapato;
h) Wakala unaandaa mfumo wa utambuzi na uthibiti wa vihatarishi -(Risk management framework).

3. MWENENDO WA MATUMIZI KATIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YA WAKALA

3.1. Mwenendo wa Matumizi Kwa Kila Lengo Kuu (Objective)

Jumla ya TSh 141,346,690,760 zimetumika kwa kipindi cha miaka minne (2011/12 – 2014/15) kutekekeleza Mpango Mkakati I wa miaka mitatu (2011/12 – 2013/14). Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2013/14, Jumla ya Shs 1,242,159,886 zilitumiwa na Wizara kwa ajili ya kutekeleza Operesheni Tokomeza. Aidha jumla ya Shs. 569,503,137 kama zilivyooneshwa kwenye taarifa ya fedha ya mwaka 2014/15 zilitumika na Wizara kwa shughuli mbalimbali kama mkopo.

Jedwali Na. 7 linaonesha muhtasari wa mwenendo wa Matumizi kwa kila Lengo Kuu kwa Mpango Mkakati I (2011/2012 - 2013/2014); na **Jedwali Na. 8** linaonesha muhutasari wa mwenendo wa Matumizi kwa kila Lengo Kuu – mwaka wa kwanza 2014/15 wa Mpango Mkakati II wa miaka mitano (2014/15- 2018/19).

Mwenendo wa matumizi katika Mpango Mkakati I unaonesha kuwa mkazo ulitiliwa katika kutelekeleza majukumu ya msingi ya Wakala, ambapo katika "**Lengo B Kuhakikisha upatikanaji wa mazao bora ya misitu na nyuki"**, matumizi yalikuwa Tshs 50,379,283,314 (50.22%) kwa ajili ya uendelezaji mashamba ya miti; kuimarisha mipaka ya misitu na kufanya tathmini ya rasilimali za misitu nchini (NAFORMA). Shughuli nyingine za kujenga uwezo na uendeshaji wa taasisi kwenye Lengo D, ikiwemo ununuzi wa magari na mitambo, ujenzi nyumba za watumishi katika mashamba na kanda; majengo ya ofisi; kuandaa mifumo ya uendeshaji; kusimamia ukusanyaji wa maduhuli na kujenga uwezo wa utendaji kazi kwa watumishi zilitumia Tshs 40,902,344,467 (40.78%) za matumizi ukilinganisha na malengo mengine.

Matumizi katika Mkakati II kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 yanaonesha kuwa Lengo C Kuimarisha uwezo wa taasisi lina matumizi ya Tshs 22,355,574,417 (48.27%) na Lengo D upatikanaji wa mazao ya misitu na nyuki na kuimarisha mifumo ikolojia lina matumizi Tshs 15,308,589,836 (33.05%) kwa umuhimu wake yakilinganishwa na malengo mengine ya Mkakati II. Maelezo ya viwango vya asilimia za matumizi vinaendelea kusisitiza kuwa Lengo C linahusu Kuendelea kujenga na Kuimarisha Mifumo ya Kiutendaji ya Taasisi ikijumuisha ununuzi wa ardhi za mashamba, viwanja, magari pamoja na vitendea kazi vingine. Lengo D linahusu usimamizi wa misitu ikijumuisha ustawishaji wa mashamba ya miti, kusafisha na kufungua mipaka, kuondoa wavamizi katika misitu na kuendeleza shughuli za ufugaji nyuki.

Jedwali Na. 7: Muhutasari wa mwenendo wa Matumizi kwa kila Lengo Kuu kwa Mpango Mkakati I (2011/2012 - 2013/2014);

DHUMUNI/ MWAKA	2011/12		2012/13		2013/14		JUMLA		% YA MATUMIZI
	BAJETI	MATUMIZI	BAJETI	MATUMIZI	BAJETI	MATUMIZI	BAJETI	MATUMIZI	
OBJECTIVE A: HIV/AIDS infections reduced and supportive services to people living with HIV/AIDS improved;	76,750,000	24,150,000	202,432,500	153,894,500	210,915,000	191,981,500	490,097,500	370,026,000	0.37
OBJECTIVE B: Sustainable supply of quality forest and bee products enhanced	13,505,604,836	15,905,929,742	12,080,350,488	11,680,734,899	24,801,454,185	22,792,618,673	50,387,409,509	50,379,283,314	50.22
OBJECTIVE C: Stable ecosystem and biological diversity maintained	4,361,314,800	1,608,563,761	4,958,086,173	3,732,016,095	4,084,413,143	2,994,713,798	13,403,814,116	8,335,293,654	8.31
D. Institutional capacity to deliver services stregthened	8,564,689,156	3,882,689,681	19,485,265,283	15,221,647,896	26,679,859,440	21,798,006,890	54,405,090,247	40,902,344,467	40.78
OBJECTIVE E: Good governance and gender balance enhanced	120,900,000	84,050,000	208,940,000	113,522,880	155,486,000	123,824,620	485,326,000	321,397,500	0.32
JUMLA	**26,629,258,792**	**21,505,383,184**	**36,935,074,444**	**30,901,816,270**	**55,932,127,768**	**47,901,145,481**	**119,171,737,372**	**100,308,344,935**	**100.00**

Jedwali Na 8: Muhutasari wa Mwenendo wa Matumizi kwa kila Lengo (Objective) – Mkakati II (Mwaka wa Fedha 2014/15)

Malengo	Makisio ya Bajeti (TSh)	Matumizi (TSh)	Asilimia ya Matumizi (%)
Lengo A;HIV/AIDS infections reduced and supportive services to staff living with HIV/AIDS improved	253,140,000	184,134,484	0.45
Lengo B: Good Governance and gender balance enhanced	2,935,138,000	3,039,099,534	7.41
Lengo C: Institutional capacity to deliver services strengthened	23,847,706,000	22,355,574,417	54.47
Lengo D: Forest and Bee Resources Base and Ecosystem Improved	14,555,293,000	15,308,589,836	37.30
Lengo E: utilisation of Quality forest and bee products enhanced	191,855,000	150,947,554	0.37
JUMLA KUU	**41,783,132,000**	**41,038,345,825**	**100.00**

3.2. Ubunifu na Mikakati ya Udhibiti wa Matumizi

a) Mchakato wa bajeti na maotea ya maduhuli unazingatia ushirikishaji katika ngazi zote za Wakala na bajeti inaandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa uandaaji wa bajeti unaotolewa na Hazina.
b) Mipango kazi inaandaliwa kwa kila kituo kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa.
c) Wakala umeanzisha mfumo wa usimamizi na udhibiti wa fedha (IFMS) kwa Makao Makuu, Shamba la Miti Sao-Hill, na Kanda ya Mashariki. Mfumo huu umeanzishwa katika vituo vinavyokusanya na kutumia fedha nyingi. Vituo vingine vitaunganishwa katika mfumo huu kwa awamu kwa kuzingatia mpango mkakati wa Wakala.
d) Wakala umeanzisha Bodi ya manunuzi kwa Makao Makuu na Bodi ndogo (Delegated tender Boards) katika vituo kwa ajili ya kusimamia manunuzi ya Wakala.
e) Wakaguzi wa ndani wa Wakala kufanya ukaguzi Makao Makuu na vituoni mara kwa mara ili kubaini kufuatwa kwa taratibu za fedha na manunuzi.
f) Wakala umenzisha Kamati ya Ukaguzi kwa ajili ya kuongeza udhibiti na uwajibikaji wa rasilimali za Wakala.

4. UTAWALA BORA NA JINSIA

a) Wakalaumetekeleza Mkakati wake wa Kuzuia na Kupambana Rushwa hadi sasa watumishi 841 katika ngazi tofauti wamepatiwa mafunzo juu ya kuzuia na kupambana na rushwa.
b) Wakala imekamilisha Mkataba wa Huduma kwa Mteja,
c) Wakala umeboresha maswala ya jinsi kwani asilimia 40 ya Wakuu wa Vitengo/

Meneja Waandamizi wa TFS Makao Makuu ni wanawake, asilimia 57 ya wasaidizi wa Meneja katika kanda za TFS ni wanawake.

5. KUPAMBANA NA JANGA LA UKIMWI NA KUTOA HUDUMA KWA WATUMISHI WANAOISHI NA HIV/AIDS

Wakala umeandaa Mkakati wa taasisi wa kupambana na HIV/AIDS mahala pa kazi. Katika kutekeleza mkakati huo, jumla ya watumishi 3,163 waWakala wa mikoa na wilaya, na wanavijiji 5,271 wamehamasishwa kuchukua tahadhari na kupimwa HIV/AIDS. kupitia warsha na semina. Watumishi 277 walipima kwa hiari. Watumishi 37 wanaoishi na UKIMWI wanasaidiwa chakula.

6. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA

Katika kutekeleza majukumu yake Wakala umepata changamoto zifuztazo:

a) Uvamizi wa maeneo ya misitu kwa ajili ya kilimo, ufugaji, makazi, ukataji miti na uchimbaji wa madini;
b) Moto katika misitu kila mwaka.
c) Sekta ya misitu na nyuki kutokuwa kipaumbele katika mipango ya maendeleo taifa;
d) Utegemezi mkubwa wa misitu kama chanzo kikuu cha nishati.
e) Pamoja na juhudi zinazofanywa naserikali za kuongeza watumishi, bado idadi ya watumishi wanao hitajika ni ndogo ukulinganisha na ukubwa wa eneo linalosimamiwa na Wakala.

7. MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

a) Kuongeza watumishi na vitendea kazi.
b) Kujenga vituo katika kila msitu wa hifadhi
c) Kuweka bayana mipaka ya hifadhi
d) Kuweka mabango yanayotoa tahadhari
e) Kuwaondoa wavamizi
f) Kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje

8. MIPANGO YA BAADAYE YA WAKALA

a) Kuwa mamlaka

Wakala umeandaa Andiko (Concept Note) la kuomba kuwa Mamlaka (Authority)

b) **Kuwa na vitega uchumi**

Wakala upo katika mchakato wa kuandaa sera ya uwekezaji (investment policy) ili kuwa na uwekezaji wa aina mbalimbali nje ya kutegemea mazao ya misitu kama chanzo kikuu cha kupata fedha.

Kiambatisho Na.1

Watumishi waliajiriwa TFS

Na	Kada	2013/14	2014/2015	2015/2016	Jumla
1.	Afisa Misitu	41	8	75	124
2.	Afisa Nyuki	10	9	20	39
3.	Msaidizi Misitu	244	83	207	534
4.	Msaidizi Ufugaji Nyuki II	16		70	86
5.	Katibu Muhtasi III	12	9	6	27
6	Afisa Utumishi II	01			1
7	Wahudumu wa masijala II	13	8	2	23
8	Maderava II	03			3
9	Walinzi	02			2
10	Wasaidizi ofisi	06	2		8
11	Mafundi mitambo	03		1	4
12	Wauguzi	02			2
13	Wataalam mifumo ya Kompyuta			2	2
14	Wachumi			2	2
15	Wahasibu wasaidizi			19	19
13	Wasaidizi Ugavi	01			1
14	Wakaguzi wandani			3	3
	Jumla	**354**	**119**	**407**	**880**

Kiambatisho Na. 2

ORODHA YA VIFAA VILIVYONUNULIWA NA TFS TOKA FBD

S/N	JINA LA VIFAA	VILIVYORITHIWA TOKA FBD	VILIVYONUNULIWA WA TFS						
			2011/2012	2012/2013	2013/2014	2014/2015	2015/2016	JUMLA VILIVYONUNULIWA NA TFS	MAONI
1	**Mitambo Mikubwa**								
	Bulldozer	5				1		1	Bulldozer 1 ni msaada toka serikali ya china
	Motor grader	4			1			1	
	Wheel Loader	3			1			1	
	Stone Crusher	1						-	
	Tractor and Trailers	16						-	
	Soil Compactor					1		1	
								-	
2	**Other working Facilities**							-	
	Generators	10				25		25	Generators 25 ni Msaada toka serikali ya china
	water pumps	2						-	
	computers	42	23	10	4	5	55	97	
	Fax Machine	3		2	1		1	4	
	Photocopier	11	3	4			9	16	
	Scaner			5	7		7	19	
	Laptop				6	26	22	54	
	Projectors			2			3	5	
	Printers			8	10	2	7	27	

	Refrigerator			2			3	5	
	Television		1				2	3	
	AFD-Machine			1				1	
	Micro wave			1				1	
3	**Furnitures and Fiiting**								
	Executive Table				6		1	7	
	office tables			16	25	7		48	
	Executive chairs/office chairs			3	10	32	64	109	
	Steel CabInet			16	7	3	8	34	
	Secretarial Chairs						15	15	
	Visitors Chairs						76	76	
	Racks						25	25	
	Conference tables								
	Transport Equipment							-	
	Lorries	26			7	3		10	
	Motor Vehicles(Station Wagon 4WD)	109		1	3	2	9	15	
	Motor vehicles Pick ups(Station Wagon 4WD)				4	25	3	32	Pick up 2 ni Msaaada kutoka Serikali ya China
	Min Bus					2		2	

	Terrain Vehicless						10	10	Terrain Vehicles ni Msaada toka Serikali ya China
	Motor cycles	83		61	200	39		300	
	Fiber Boat	5				1		1	
	Building & Structures								
	Office Building	63			3	1	3	7	
	Residential Buildings	580			2	9		11	
	Workshops & Garages	23						-	
	Dispensaries	9						-	
	Social Hall/ Facilities	12				1		1	
	Stores	7						-	